Taarifa Fupi

Maswali ya Mara kwa Mara

Kuhusu Microbicides

***Microbicides* ni nini?**

(Mī-KRO'-bĭ-sīdz) *Microbicides* ni aina mpya ya bidhaa ambazo zinayotengezwa ili watu waweze kutumia ndani ya sehemu ya uzazi ya mke au ndani ya sehemu ya haja kubwa ili kujikinga dhidi ya virusi vya UKIWMI na labda hata pia magonjwa mengine ya ngono. Microbicides zinaweza kutengezwa kwa namna tofauti, ikiwemo jeli, krimu,tembe za kuingiza ndani ya sehemu ya uzazi ya mke, utandu, mafuta au kupelekwa kwa njia ya sponji au mviringo wa uke ambao hutoa viungo vinavyofanya kazi pole pole.

***Microbicides* zitapatikana lini?**

Wanasayansi wanafanyia bidhaa nyingi majaribio ili waone kama zitaweza kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI na/au magonjwa mengine ya ngono, lakini kwa sasa hakuna *microbicide* iliyo salama na ambayo imethibitishwa kuwa inazuia virusi vya UKIMWI, inayopatikana kwa matumizi ya uma. Wanasayansi wanafuatilizia kwa uzito tangulizi nyingi za bidha hii, ikiwepo kadhaa ambazo zimethibitishwa kuwa salama na zenye kukinga virusi vya UKIMWI katika majaribio na wanyama, na ambazo sasa nizafanyiwa majaribio kwa binadamu (majaribio ya zahanati). Ni vigumu kusema itachukuwa mda gani kupata *microbicide* iliyo salama na yenye kinga. Kwa kadiri, utengezaji wa dawa mpya huchukua zaidi ya mwongo mmoja (miaka kumi) kutoka kubainika kwenye maabara ya utafiti hadi kupatikana kwa soko. Asilimia tisini ya aina za bidhaa ambazo hufanyiwa utafiti kwenye maabara, hutupiliwa mbali hata kabla ya kuingia kwenye majaribio ya zahanati. Ni aina chache tu za bidhaa za *microbicides* ambazo zimefikia ngazi za mwisho za majaribio kuona kama ziko na uwezo wa kuzuia virusi vya UKIMWI (haya majario yanaweza kuchukua hadi miaka mine). Matokeo ya jaribio la ngazi ya IIb la CAPRISA 004 katika nchi ya Africa Kusini limetoa onyesho kwamba jeli ya kutumia katika njia ya uzazi ya mke iliyotengenezwa na dawa za kuzuia makali ya virusi vya UKIMWI yaweza kuzuia uwezekano wa kwambukizwa. Jaribio la siku za usoni likaonyeshana kwamba Tenofovir—au bidhaa yoyote nyingine iliyo/itakayotafitiwa—inazuia virusi vya UKIMWI, itakuchua kati ya miaka miwili hadi minne kwa nchi binafsi kusajili *microbicides* kwa matumizi ya uma. Kwa sababu ya hizi fumo tofauti kati ya mataifa, microbicides hazitapatikana kwa nchi zote kwa wakati mmoja, na pia sio watu wote katika nchi wataipata kwa wakati mmoja. Yamkini, kwa wakati wa mwanzo, zitazitapatikana na watu wachache, ingiwa kila nchi itaendelea kuongezea upatikanaji. Kwa mfano, uwezo wa kukinga maambukizi kwenye wanawake utaweza kuthibitishwa kabla ya wanaume, kwa maana, majaribio ya ngazi za juu katika binadamu, yamelenga matumizi ya njia ya uzazi ya mke hadi sasa.

***Microbicides* zitafanya kazi vipi?**

Microbicides zinaweza kufanya kazi kwa njia tofauti kama vile kuangamiza kukomaa kwa virusi vya UKIMWI kabla au baada ya kuingia katika chembechembe za damu, au pia kuzuia virusi kujiambatisha na chembechembe za CD4. Bidhaa zingine za microbicides hulenga virusi vya UKIMWI pekee na zingine hulenga virusi vya aina mbalimbali vya majonjwa ya ngono vikiwemo vile vya UKIMWI).

Je, *microbicides* zitaondoa haja ya kondomu?

La. Zikitumika kila wakati na kwa usahihi, kondomu za kiume au kike zaweza peana kinga bora dhidi ya virusi vya UKIMWI na magonjwa ya ngono kuliko *microbicides*, kwa hivyo zitaendelea kuwa chaguo muhima katika kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Lakini kwa watu ambao hawawawezi au hawatatumia kondomu, na haswa kwa wanawake ambao wapenzi wao hukataa kondomu, utimiaji wa *microbicides* utaokoa maisha na utachangia kwa pakubwa kuzuia usambazaji wa virusi vya UKIMWI.

Je, kama mwanamke anataka kupata mimba?

Bidhaa za *microbicides* zote ambazo zimo katika ngazi za juu za majaribio kwa sasa, hazina uwezo wa kuzuia mimba. Katika siku za usoni, wanawake wataweza kupata aina tofauti za *microbicides,* zile ambazo haziwezi kuzuia kupata mimba and pia zenye uwezo wa kuzuia kupata mimba. *Microbicides* zenye vidonge vya kuzuia mimba zitakimu mahitaji mawili kwa wanawake ambao wanalenga kuzuia kupata mimba na pia kujikinga tukotakana na maambukizi ya virusi UKIMWI au magonjwa ya ngono kwa kutumia bidhaa moja. Bidhaa ya *microbicide* isiyo na uwezo wa kuzuia kupata mimba ikishaguduliwa, kuna uwezekano wa kuongezea vidonge vya kuzuia kupata mimba.

Je, *Microbicides* zitaweza kinga dhidi ya magonjwa yote ya ngono?

Ingawa kinga dhidi ya virus vya UKIMWI ndio lengo kuu, tunatumaini kuwa *microbicides* ambazo zinauwezo wa kukinga dhidi ya magonjwa mengine ya ngono pamoja na virusi vya UKIMWI zitaweza kupatikana siku za usoni. Utafiti wa matumizi ya geli iliyo tengenezwa na dawa ya 1% Tenofovir kwenye sehemu ya uzazi ya mke ulionyesha kwamba yaweza pia kinga maambikizi ya virusi vya *herpes simplex* aina ya pili *(HSV-2).*

Je *Microbicides* zitakuwa salama?

Bidha yoyote mpya lazima ipitie upimaji wa hali ya juu kuhakikisha kwamba haina madhara kwa binadamu na pia idhinishe na serikali kwa matumizi ya uma. Wanaharakati wa afya ya wanawake na watafiti wanashirikiana kuhakikisha kwamba utafiti wa *microbicides* unafanywa kwa umakini na uadilifu. Kwa ubahati, nyingi za bidhaa za microbicides ambazo ninafanyiwa utafiti ni dawa ambazo tayari zinatumika kwa matibabu.

Je, wanaume watafaidi kutokana na *microbicides* pia?

Ingawaje inawezekana kuwa *microbicides* zinaweza kinga washiriki wa ngono wa wanawake walio na virusi vya UKIMWI, pia inawezekana kuwa hazitaweza. Ni muhimu majaribio kwa wapenzi ambao hali yao ya maambiki ya virusi vya UKIMWI inatofautiana yafanyike ili hili jambo lieleweke. Utafiti wa *microcides* za kutumia kwenye njia ya haja kubwa unaendelezwa. Usalama na uwezo wa microbicides kuzuia maambuziki zikitumiwa kwa njia ya haja kubwa ni lazima uthibitiswe tafauti na matumizi ya njia ya uzazi ya mke.

Ni nani anafanya kazi kwenye utafiti na ubuni wa *Microbicides*?

Karibu utafiti wote wa *microbicides* amabo uendelezwa hadi sasa, umefanywa na mashirika yasiyo ya kifaida na taasisi za elimi au kampuni ndogo za utafiti wa dawa. Huu utafiti wa kubuni *microbicides* hufadhiliwa na wakfu za kibinafsi na fedha za kiserikali. Hizi fedha za uma pia zinafadhili utafiti wa kimsingi wa sayansi, utafiti wa kijamii na kitabia, na miundobinu ya majaribio kwenye binadamu. Kampuni kubwa za madawa hazija changia kwa ukubwa katika nyanja hii. Hii sana sana ni kwa sababu faida kutokana na mauzo ya *microbicides* yanatarajiwa kuwa duni. Hizi kampuni kubwa za madawa zimechangia kwa kutoa idhini ya madawa yao kutumiwa katika utafiti wa njia mpya za kukinga maambukizi.

Mbona tunahitaji *microbicides* ikiwa hapo mwishowe tutakuwa na chanjo ya virusi vya UKIMWI?

Hakuna mkakati au teknolojia ambayo "itatatua" mlipuko wa ugonjwa wa UKIMWI ikiwa peke yake. Ni lazima tutumie mikakati yote iliyoko ya kuzuia maambukizi – kama ubadilishaji wa tabia, ushaururi na upimaji wa hiari, uaguzi na matibabu ya magonjwa ya ngono, upanuzi wa matumizi ya kondomu za kiume na kike, kupatikana kwa sindano karema *(sterile needles and syringes)*, na matumizi ya dawa za kupunguza makali – na pia kupanua aina za bidhaa na teknolojia zinazo hitajika kwa kukinga na matibabu ya virusi vya UKIMWI. *Microbicides* zinawezekana kugunduliwa na kusambazwa karibuni chanjo ya virusi vya UKIMWI. Hata baada ya uvumbuzi wa chanjo salama na kamilifu, chanjo na *microbicides* zitakimu mahitaji tofauti, katika kukinga maambukizi.

Microbicides zitagharimu pesa ngapi, na watu wataweza kuzigharamia?

Ni muhimu kwamba microbicides zifike kwenye mikono ya wanawake na wanaume wanaozihitaji kwa bei wanoyoweza kugharamia. Hapo awali, teknolojia mpya za kiafya hazikuweza kupatikana kwa urahisi katika nchi zinazoendelea kwa muda wa zaidi ya mwongo mmoja baada ya kugundulia na kusajiliwa katiaka nchi za Kazkazini. Hali hii haitakubalika kwa hii teknolojia muhimu ya kuokoa maisha, hususani kwa kuwa bidhaa za kuzuia virusi vya UKIMWI zimebuniwa haswa na fedha za uma kwa matumizi katika maeneo yaliyoadhirika zaidi. Wanaharakati wanashirikiana na watafiti pamoja na serikali mbalimbali ili kutilia mkazo umuhimu wa kubuni mikakati ya kuhakikisha kwamba wakati tu *microbicides* zilizo salama na kamilifu zitakapoguduliwa, njia za kugharamia na pia usabazaji zitakutuwa zimetayarishwa. kutatua mambo ya kupata na kugharimia kwanza , ili kuwa tayari kukabidhi microbicides haraka mara tuu inapothibitishwa kuwa salama na kamilifu.

Unaweza kujihusisha kivipi?

Tembelea tovuti ya Kampeni ya Kidunia ya *Microbcides* (Global Campaign for Microbicides) (www.global-campaign.org) kuweka sahihi kwenye mwito kwa washirikadau, jiandikishe kupokea habari, mwandikie mbunge wako barua, kukutana na vikundi vya wanaharakati katika eneo lako, na pia ujifunze mengi zaidi kuhusu *microbicides*. Tunahitaji usaidizi wako kuwezesha *microbicide* iliyo salama na inayozuia maambukizi kupatikana kwa haraka iwezekanavyo.

Kampeni ya Kidunia ya *Microbicides* (Global Campaign for Microbicides - GCM) ni asasi ya kijamii inayofanya kazi kuhakikisha kwamba utafiti wa njia mpya za kukinga maambukizi ya virusi vya UKIMWI, pamoja na usambazaji wa hizi njia mpya pamoja na zinazotumika kwa sasa – hasa kwa wanawake, unafanyika kwa hali ya uadilifu.

Tembelea Tovuti: www.global-campaign.org au tuma barua pepe: info@global-campaign.org

Kampeni ya Kidunia ya M*Microbicides* (Global Campaign for Microbicides). 2011. Uchapishaji na usambazaji wa nakal hii unahimizwa.
Kwa maelezo zaidi wasiliana na: info@global-campaign.org Kupata toleo jipya tembelea: www.global-campaign.org/download.htm.